# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| DIBAJI | 1 |
| UTANGULIZI | 2 |
| MWONGOZO WA WAKUFUNZI KUHUSU USAWA WA KIJINSIA | 3 |
| MADA YA KWANZA: USAWA WA KIJINSIA NCHINI TANZANIA | 4 |
| MADA YA PILI: SHERIA NA SERA ZA KITAIFA JUU YA USAWA WA KIJINSIA | 9 |
| MADA YA TATU: UBAGUZI WA KIJINSIA | 12 |
| MADA YA NNE: UKATILI WA KIJINSIA | 19 |
| MADA YA TANO: DHANA ZA MSINGI KUHUSU UWEZESHWAJI WA WANAWAKE NA WASICHANA | 24 |
| MADA YA SITA: AINA ZA UWEZESHWAJI WA WANAWAKE NA WASICHANA | 26 |



# DIBAJI

**Uwezeshaji kupitia Ujuzi (ESP)** ni mradi wa miaka 7 (2021-2028) unaotekelezwa na Jumuiya ya Vyuo na Taasisi za Ufundi Kanada (CICan) kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Tanzania (WyEST) kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (DTVET). Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Kanada.

Lengo kuu la mradi ni ***kuboresha ushiriki wa wanawake na wasichana kwenye shughuli za kiuchumi nchini Tanzania.*** Mradi huu unafanya kazi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) na Asasi za Kijamii (CBOs) katika wilaya 12 nchini Tanzania, ukilenga kuongeza viwango vya ushiriki kwa wanawake na wasichana katika programu za mafunzo ya ujuzi na kuboresha upatikanaji wa mafunzo ya biashara, ujuzi, jinsia na haki za binadamu katika jamii zetu.

In partnership with Canada | Colleges & Institutes Canada

collegesinstitutes.ca

# UTANGULIZI

Uwezeshaji kupitia Ujuzi (ESP) ni mradi unaolenga Usawa wa Kijinsia kulingana na Sera ya Msaada wa Kimataifa ya Kanada (FIAP). Hivyo, matokeo ya mradi katika ngazi zote yanalenga kushughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia ili kuendeleza ushiriki katika kufanya maamuzi.

FIAP ilizinduliwa mnamo Mwaka 2017. Kupitia FIAP, Kanada inatoa asilimia 95% ya misaada yake ya kimataifa ili kuzingatia usawa wa kijinsia na uwezeshaji.

# TAHADHARI

Mwongozo huu unajumuisha michoro yenye maudhui inayolenga kuwasaidia wasomaji kuelewa somo husika hata hivyo kuna uwezekano wa michoro hiyo kuzua hisia au kutafsiriwa visivyo na kusababisha maudhi kwa baadhi ya wasomaji. Hivyo, busara ya msomaji inashauriwa.

# MWONGOZO WA WAKUFUNZI KUHUSU USAWA WA KIJINSIA

Kitabu hiki kina mada sita na kitatumika kama zana ya wakufunzi itakayosaidia mchakato wa kuelimisha hadhira lengwa kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia, athari za kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia, na kutambua mipango ya kufikia usawa wa kijinsia ili kukidhi jamii kwa ujumla.

Dhamira kuu ya mafunzo haya ni kupunguza vizuizi vyote vya kufikia au kufaidika na usawa wa kijinsia nchini Tanzania.

## Zana na Mbinu za Mafunzo


Ili kufikia malengo ya mwongozo huu, wakufunzi watatumia zana na mbinu zitakazowezesha uwasilishaji wa mada mbalimbali zinazohusiana na usawa wa kijinsia.

## Zana za Mafunzo

Picha, chati, kadi za manila, kalamu za rashasha, nukuu za mkufunzi, dodoso, nakala za sheria na sera za kitaifa.







## Mbinu za Mafunzo


Mhadhara shirikishi, kazi za vikundi na bungua bongo




# MADA YA KWANZA:
# USAWA WA KIJINSIA NCHINI TANZANIA

Jinsia ni nafasi na majukumu maalumu yaliyotengenezwa na jamii kwa ajili ya wanaume na wanawake.


Usawa wa kijinsia unamaanisha kuwa wanaume na wanawake wana nafasi na fursa sawa kwenye masuala ya kujitegemea kiuchumi, kifedha, kielimu na kujiendeleza.






Usawa wa kijinsia unahusiana na kuwatendea bila upendeleo wanawake na wanaume kadri ya mahitaji yao binafsi. Hii inamaanisha kwamba, kila jinsi inawakilishwa sawia kwenye kundi fulani.

### Alama za Usawa wa Kijinsia Barani Afrika – 2019 (Chanzo: Statista)




*Alama 1 inaashiria kufikiwa kwa Usawa wa Kijinsia*

Mchoro huu unaonesha kwamba, kati ya nchi za Kiafrika zilizotajwa hapo juu hakuna iliyofikia usawa wa kijinsia. Na hii ni kulingana na alama 1 ambayo inamaanisha kwamba usawa wa kijinsia umefikiwa.

## Malengo ya Mada:

Baada ya kumaliza mada hii, kila mshiriki ataweza:

a) Kutathmini usawa wa kijinsia nchini tanzania.
b) Kujenga utayari wa kushiriki kikamilifu kwenye ufuatiliaji wa usawa wa kijinsia kwenye jamii zetu na nchini Tanzania.

## Utangulizi

Mkufunzi atawaongoza washiriki kuandika matarajio kuhusu mada itakayofundishwa.


## Tathmini/Kazi ya Awali

Mkufunzi atawaongoza washiriki kujadili na kutoa tathmini ya awali ya usawa wa kijinsia nchini Tanzania.

## Uwasilishaji

1) Washiriki watawasilisha majibu ya kazi za vikundi.
2) Mkufunzi ataonesha filamu au kusoma taarifa fupi ya usawa wa kijinsia nchini Tanzania.

### Kielelezo cha Pengo la Usawa wa Kijinsia Ulimwenguni (2022), kwa Mgawanyiko wa Kikanda (Chanzo: Ripoti ya Pengo la Kijinsia Duniani 2022)




**Kwa kasi ya sasa ni lini maeneo haya yataweza kuziba pengo?**

## Mazoezi
Washiriki watatoa tathmini fupi za usawa wa kijinsia kwenye jamii zetu.

## Upimaji na Tathmini Baada ya Mafunzo
Mkufunzi atatathmini ubora wa taarifa fupi zilizowasilishwa na washiriki na kuuliza maswali ya kupata ufafanuzi.

## Tafakari
Mkufunzi atawaongoza washiriki kutafakari athari na hatua za kuchukuliwa kutokana na hali ya usawa kijinsia iliyopo kwenye jamii zetu na taifa kwa ujumla.

## Hitimisho
Mkufunzi atatoa muhtasari mfupi wa mada zilizofundishwa, na kujibu maswali yoyote kutoka kwa washiriki. Mwishoni atahitimisha mada.


| Nukuu za Mkufunzi |
|---|
| **Usawa wa Kijinsia nchini Tanzania** |
| ✓ Usawa wa kijinsia umefikiwa kwenye elimu ya msingi. |
| ✓ Katika taasisi za elimu pia, wanawake wanashikilia nafasi za juu za uongozi kwa mfano: Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari, Waratibu Elimu n.k. |
| ✓ Katika ngazi mbalimbali za serikali za mitaa, wanawake wameshikilia nyadhifa mbalimbali kama vile: Wakurugenzi wa Miji, Wakuu wa Wilaya, Watendaji Kata, Wenyekiti wa Mitaa n.k. |
| ✓ Tanzania imefanikiwa kuwa na Rais wa kwanza mwanamke ambaye ni Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. |
| ✓ Nafasi za juu za Serikalini ikiwemo nafasi ya Spika wa Bunge kwa sasa inashikiliwa na mwanamke ambaye ni Mhe. Dkt. Tulia Ackson |
| ✓ Wanawake wapo kwenye ngazi za juu kwenye makampuni, mathalani: Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB ambayo ni kati ya benki kubwa za Kitanzania ni mwanamke (Bi. Ruth Zaipuna). |




## Usawa wa Kijinsia nchini Tanzania (Changamoto)

- ✓ Idadi ya wanawake kwenye elimu ya juu bado ni ndogo.
- ✓ Idadi ya wanawake kwenye nafasi za siasa na maamuzi bado ni ndogo.
- ✓ Uviko-19 umeongeza hali ya ukatili wa kijinsia na manyanyaso kwa wanawake.
- ✓ Unyanyasaji wa kijinsia bado unaendelea hasa wakati wanawake wana sifa za kupandishwa vyeo au kwenye usalama wa kazi.
- ✓ Asilimia chache ya wasichana ndio wanaomaliza masomo ya sekondari na vyuo ukilinganisha na wavulana.
- ✓ Wanawake wachache wanashikilia nafasi za juu za uongozi za kitaifa (Wizarani, Bungeni, na kadhalika).
- ✓ Ubaguzi wa kijinsia hasa kwenye sheria za kimila katika maeneo ya vijijini bado unaendelea kujitokeza.
- ✓ Idadi ya wanawake katika fursa za ajira ni ndogo na wengi wanafanya kazi katika sekta zisizo rasmi (wanawake wanabaguliwa kwenye fursa za ajira kutokana na sifa za kibaiolojia mfano: kubeba ujauzito, na kutokana na mgawanyo wa majukumu kati ya wanawake na wanaume kwenye jamii

Hapa chini ni taarifa rasmi inayosaidia kuelezea muelekeo wa usawa wa kijinsia nchini Tanzania. Takriban asilimia 60% ya wanawake wanaishi katika umaskini uliokithiri Wanawake wapatao asilimia 70% ndio nguvu kazi ya kilimo, hata hivyo ni asilimia 9% tu ndio wanamiliki ardhi.




Vile vile ni asilimia 12% tu wanaotumia huduma za kibenki. Pia wanawake hutumia muda mara tatu (3*) zaidi ya wanaume kufanya kazi za utunzaji wa ndani bila malipo (Uchambuzi kutoka Mkakati wa Usawa wa Kijinsia – Mradi wa ESP).

Mnamo Julai 2021 Serikali iliungana na viongozi ulimwenguni ili kutoa ahadi za kuharakisha maendeleo ya usawa wa kijinsia kwa kushirikiana na Muungano wa Utekelezaji wa Jukwaa la Usawa wa Haki za Kiuchumi

Tanzania imedhamiria kufikisha ahadi hiyo ifikapo mwaka 2026 kwa kulenga kwenye uwekezaji wa huduma bora za kijinsia kwa umma na binafsi; kwa kujenga mazingira wezeshi ya kisheria na kisera ili kupelekea uongezekaji wa kazi nzuri kwa wanawake katika uchumi rasmi au usio rasmi; kwa kupanua upatikanaji wa rasilimali zenye tija; na kubuni na kutekeleza vichocheo vya uchumi vinavyozingatia jinsia ili idadi ya wanawake na wasichana wanaoishi kwenye umaskini ipungue.

# MADA YA PILI:

# SHERIA NA SERA ZA KITAIFA JUU YA USAWA WA KIJINSIA

## Malengo ya Mada:

Mara baada ya kumaliza mada hii, kila mshiriki ataweza:

a) Kutambua sheria na mikataba ya kitaifa ya kuleta usawa wa kijinsia.
b) Kuelezea kwa ufupi ibara zinazohusiana na haki za wanawake.

## Utangulizi

Mkufunzi atawaongoza washiriki kuandika matarajio yao kuhusu mada itakayofundishwa.

## Tathmini/Kazi ya Awali

Mkufunzi atawataka washiriki wataje sheria na sera za kitaifa wanazozifahamu kuhusu ulinzi wa haki za binadamu na wanawake kwa kipekee.

## Uwasilishaji

1) Mkufunzi ataorodhesha sheria na sera za kitaifa za kukuza usawa wa kijinsia.
2) Mkufunzi ataelezea kwa ufupi maudhui ya sheria na sera za kitaifa za kukuza usawa wa kijinsia.

## Mazoezi

Mkufunzi atawaongoza washiriki kujadili kuhusu utekelezaji wa sheria na sera za kitaifa za kukuza usawa wa kijinsia kwenye jamii zetu na Tanzania kwa ujumla.

## Upimaji na Tathmini Baada ya Mafunzo

Mkufunzi atawaongoza washiriki kwa njia ya maswali; wataje sheria na sera za kitaifa za kukuza na kutetea usawa wa kijinsia.

## Tafakari

Mkufunzi atawaongoza washiriki kutafakari umuhimu wa sheria na sera za kitaifa kwa ajili ya kutetea usawa wa kijinsia kwenye mazingira ya Kitanzania na katika jamii zetu.

## Hitimisho

Mkufunzi atatoa muhtasari mfupi wa mada zilizofundishwa, na kujibu maswali yoyote kutoka kwa washiriki. Mwishoni, atahitimisha mada.

## Nukuu za Mkufunzi

### Sheria na Sera za Kitaifa za kukuza Usawa wa Kijinsia

Kuna sheria na sera mbalimbali za kitaifa za kukuza usawa wa kijinsia nchini tanzania. Sheria na sera hizo ni pamoja na:

- ✓ Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- ✓ Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia
- ✓ Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Jinsia

## 1. KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Ufafanuzi:** Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa mwaka 1977, na ndio chombo mama cha ulinzi wa haki za binadamu kwa raia wote wa Tanzania.

**Wasifu:** Ibara mbalimbali za Katiba zimetoa maana, mipaka na aina ya uhuru, haki na wajibu wa raia kama ifuatavyo:

- → Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.
- → Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.
- → Kila mtu ana haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi kwa mali yake kwa mujibu wa sheria.

**Changamoto zake:**

Sera imetambua kuwa hali ya wanawake bado hairidhishi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:

- → Mila na desturi zinazowabagua wanawake.
- → Tafsiri potofu ya dhana ya wanawake kwenye maendeleo.
- → Mgawanyo usio wa haki wa rasilimali.

## 2. SERA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA JINSIA

**Ufafanuzi:** Nchi ya Tanzania inaamini katika usawa na haki kwa kila mtu kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 1992 iliundwa ili kukabiliana na changamoto zilizoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Wasifu:** Malengo ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni pamoja na:

- → Kutoa tafsiri sahihi ya dhana ya wanawake kwenye maendeleo.
- → Kuhakikisha ushiriki kamili wa wanawake katika mipango ya maendeleo ya taifa ili kutumia kikamilifu vipawa na uwezo wao.

**Changamoto zake:**

- → Ukosefu wa mipango madhubuti ya kuwawezesha wanawake kuongeza uwezo, utaalamu na ujuzi wa kutekeleza majukumu yao.
- → Ukosefu wa chombo maalum chenye jukumu la kutunga na kutoa miongozo na kufuatilia utekelezaji wa programu za maendeleo kwa wanawake.

**(Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum).**

## 3. MKAKATI WA KITAIFA WA MAENDELEO YA KIJINSIA

**Ufafanuzi:** Lengo kuu la Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia (2005) ni kufikiwa kwa usawa wa kijinsia nchini Tanzania kama ilivyobainishwa kwenye Katiba na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia.

**Wasifu:** Maeneo muhimu yaliyoainishwa kwenye mkakati huu ni pamoja na mifumo ya kitaasisi, uongozi na vyombo vya maamuzi, haki za kisheria na za kibinadamu, elimu na mafunzo, ajira, uwezeshwaji wa kiuchumi, mgawanyo wa majukumu, ujumuishaji wa kijinsia, mila na desturi na kadhalika.

Baadhi ya mikakati iliyopo kwenye Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia ni pamoja na:

- → Kuwawezesha na kuwasaidia wanawake kwenye ushiriki wa kisiasa na kugombea nafasi za uongozi.
- → Kubuni na kuweka mifumo ya kuwasaidia wanawake na wanaume kwenye masuala ya kitaaluma na fani.
- → Kuhakikisha kuna upatikanaji wa zana za kufundishia na za kujifunzia zinazozingatia jinsia.
- → Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake na kuwawezesha kupata masoko mazuri.

# MADA YA TATU:
# UBAGUZI WA KIJINSIA

Ubaguzi wa kijinsia ni mitazamo ya kijumla kuhusu sifa, tabia, majukumu au tofauti kuhusu jinsia fulani.

Kutokana na ufafanuzi huo; mkufunzi atawapa nafasi washiriki kujiunga katika makundi makubwa machache, na kushiriki katika maigizo mafupi na ya kibunifu yatakayoonesha viashiria vya ubaguzi wa kijinsia katika jamii walizotoka.

## Malengo ya Mada

Mara baada ya kumaliza mada hii, kila mshiriki ataweza:

a) Kueleza maana ya ubaguzi wa kijinsia.
b) Kufafanua aina mbalimbali za ubaguzi wa kijinsia.
c) Kutambua aina mbalimbali za ubaguzi wa kijinsia zinazowakabili wanawake na wasichana.

## Utangulizi

Mkufunzi atawaongoza washiriki kuandika matarajio yao kuhusu mada itakayofundishwa.

## Tathmini/Kazi ya Awali

1) Mkufunzi ataonesha picha za fani mbalimbali.
2) Mkufunzi atawaongoza washiriki kujaza dodoso linaloonesha kazi zinazoendana na kila jinsi.
3) Mkufunzi atawaongoza washiriki kujadiliana kwenye vikundi maana na aina za ubaguzi wa kijinsia.

## Uwasilishaji

1) Washiriki watawasilisha majibu kutoka kwenye majadiliano ya vikundi.
2) Mkufunzi ataongoza majadiliano mafupi na kuongeza maarifa ya ziada yanayohusu ubaguzi wa kijinsia.

## Mazoezi

Washiriki watakaa katika jozi na kuelezana kwa zamu maana na aina za ubaguzi wa kijinsia.

## Upimaji na Tathmini Baada ya Mafunzo

Mkufunzi atawapatia tena washiriki dodoso la mwanzo la kujaza jinsi kwa kila aina ya kazi ili kupima mabadiliko ya mitazamo kwa washiriki.

## Tafakari

Mkufunzi atawaongoza washiriki kutafakari kuhusu visababishi vya ubaguzi wa kijinsia dhidi ya wanawake.

## Hitimisho

Mkufunzi atatoa muhtasari mfupi wa mada zilizofundishwa, na kujibu maswali yoyote kutoka kwa washiriki. Mwishoni, atahitimisha mada.

### Nukuu za Mkufunzi


#### Ubaguzi wa Kijinsia

Ubaguzi wa kijinsia ni mitazamo na tabia ambazo zinahusianishwa na kuwepo kwa wanaume au wanawake. Ubaguzi wa kijinsia unaweza kuwa chanya au hasi.

Chimbuko la ubaguzi wa kijinsia ni tamaduni na mila. Watoto hujifunza tabia zipi ni za wanaume na za wanawake kutoka kwenye familia, marafiki, vyombo vya habari na taasisi mbalimbali kama shule na taasisi za kidini.


#### Mtazamo wa jamii kuhusu wanaume

- ✓ Wanaume ni wakakamavu na wana nguvu
- ✓ Wanaume hawana hisia wala huruma
- ✓ Wanaume wanaongozwa na fikra na akili
- ✓ Wanaume ni waoga kuingia kwenye mahusiano
- ✓ Wanaume wanavutiwa zaidi na kazi na majukumu yao
- ✓ Wanaume hawana hamu ya kuingia kwenye ndoa na kufanya majukumu ya uzazi




| | Mtazamo wa jamii kuhusu wanawake |
|---|---|
| | ✓ Wanawake hawana lolote, na ni kama watoto |
| | ✓ Wanawake wanaongozwa zaidi na hisia na huruma |
| | ✓ Wanawake hawana utulivu wala uwezo wa kufikiria |
| | ✓ Wanawake wanaweza kutengeneza kwa urahisi muunganiko wa kihisia |
| | ✓ Wanawake hawavutiwi na kazi |
| | ✓ Wanawake wanavutiwa na mahusiano ya muda mrefu na majukumu ya uzazi |








Ubaguzi wa kijinsia ni kumtendea mtu vitendo vibaya kutokana na jinsia yake. Wanawake na wasichana ndio mara nyingi hukumbana na athari mbaya za ubaguzi wa kijinsia kuliko wanaume.


| | Mifano ya Ubaguzi wa Kijinsia |
|---|---|
| | ✓ Kunyimwa nafasi ya kupata elimu |
| | ✓ Kuwa na hadhi ya chini kwenye jamii |
| | ✓ Uhuru mdogo wa kufanya maamuzi binafsi na yanayohusu familia |
| | ✓ Malipo/ujira mdogo kuliko kazi wanazofanya |
| | ✓ Kuwa hatarini kukumbwa na ukatili na manyanyaso |


KAZI SAWA
MALIPO
MALIPO




STOP!
HUNA MAAMUZI
HUMU NDANI!
LAKINI...!
!
!

## SHUGHULI: OANISHA AINA YA KAZI NA JINSI (WEKA ALAMA YA () SEHEMU HUSIKA)

| Picha zinazotambulisha majukumu au aina fulani ya kazi | Inafaa kwa wanaume | Inafaa kwa wanawake | Inafaa kwa jinsi zote |
|---|---|---|---|
|  | | | |
|  | | | |
|  | | | |
|  | | | |
|  | | | |

## Nukuu za Mkufunzi

### Aina mbalimbali za Ubaguzi wa Kijinsia

***a) Haiba/Tabia***

Wanawake huwa wanategemewa kuonesha tabia ya kukubaliana na kila jambo, kuonesha hisia waziwazi na wenye aibu, wakati wanaume ni wenye vurugu na wanapaswa kujiamini.

***b) Majukumu ya Nyumbani na Familia***

Jamii hutegemea mwanamke afanye majukumu ya kulea watoto, kupika, kufanya usafi na kazi nyingine za nyumbani. Kwa upande wa pili, jamii hutegemea mwanaume kutafuta fedha, kushughulika na gari na kufanya ukarabati wa hapa na pale.

***c) Kazi***


Watu wengi hudhania kwamba kazi flani zinafaa jinsi flani mfano kazi za ualimu na unesi ni za wanawake wakati kazi za urubani, udaktari na uhandisi ni maalum kwa ajili ya wanaume.

Katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi, wanawake ndio wachuuzi (wauzaji wadogo wadogo wa samaki), na wanaume ni wavuvi wa samaki. Pia wakulima wa mwani kwa asilimia kubwa ni wanawake. Mifano hii ni dhahiri kwamba jinsi zote zinaweza kufanya kazi tofauti.


***d) Muonekano wa Nje***

Mwanamke anatarajiwa kuwa na muonekano wa wembamba na nyororo, wakati mwanaume anatarajiwa kuwa ni mrefu na mwenye misuli. Hali kadhalika, wanaume na wanawake wanapaswa kuvaa mavazi ambayo ni rasmi kwa kila jinsi.





**Tafakari:**
Mkufunzi anaweza kutoa mifano ya ubaguzi wa kijinsia kutoka kwenye jamii husika ambayo ni rahisi kufahamika.




Mada hii inaweza kuhitimishwa kwa kuweka nukuu kutoka wanawake waliofanikiwa katika ngazi mbalimbali pasipokukwamishwa na mawazo ya jamii kuhusu uwezo wao.

***Mfano wa Kwanza (Nukuu:)***

***"Nawapongeza wanawake wote kwa mchango wenu adhimu katika ujenzi wa Taifa. Tuendelee kuunga mkono jitihada zinazolenga kumkomboa mwanamke kwani, maendeleo ya kweli ni yale yenye mazingira bora kifursa kwa wote".*** Alisema Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, 2023.

***Mfano wa Pili (Nukuu:)***

***"Hakuna nchi inayoweza kustawi ikiwa itakandamiza uwezo wa wanawake wake na kujinyima michango ya nusu ya raia wake. Hakuna kikomo kwa kile sisi, kama wanawake, tunaweza kutimiza".*** – Mke wa rais wa zamani wa Marekani, Michelle Obama.

Pia washiriki wa mafunzo haya watapewa nafasi ya kutaja watu ambao ni mifano ya kuigwa kwa upande wao.

# MADA YA NNE:
# UKATILI WA KIJINSIA

Ukatili wa kijinsia ni ukatili anaotendewa mtu kutokana na jinsi yake.

Katika hatua za kupambana na ukatili wa kijinsia; Tanzania imeweka mikakati kadhaa ya kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake ikiwa ni pamoja na Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Tanzania kwa miaka 2017/18-2021/22.

### Malengo ya Mada:
Mara baada ya kumaliza mada hii, kila mshiriki ataweza:

a) Kubaini maana ya ukatili wa kijinsia.
b) Kubaini na kufafanua aina mbalimbali za ukatili wa kijinsia.
c) Kutambua na kuelezea athari za ukatili wa kijinsia.

### Utangulizi
Mkufunzi atawaongoza washiriki kuandika matarajio yao kuhusu mada itakayofundishwa.

### Tathmini/Kazi ya Awali
Mkufunzi atawaongoza washiriki kubungua bongo kuhusu maana, aina na athari za ukatili wa kijinsia.

### Uwasilishaji
1) Washiriki watawasilisha majibu waliyopata kutoka kwenye majadiliano ya vikundi.
2) Mkufunzi atafafanua na kuongezea maelezo ya ziada kuhusu mambo muhimu yanayohusiana na maana, aina na athari za ukatili wa kijinsia.

### Mazoezi
Washiriki watajadili ni kwa kiwango gani ukatili wa kijinsia unazorotesha juhudi za kufikiwa kwa usawa wa kijinsia.

### Upimaji na Tathmini Baada ya Mafunzo
Mkufunzi atauliza maswali kwa washiriki.

### Tafakari
Mkufunzi atawaongoza washiriki kutafakari mafanikio na changamoto za kupambana na ukatili wa kijinsia katika jamii zao.

### Hitimisho
Mkufunzi atatoa muhtasari mfupi wa mada zilizofundishwa, na kujibu maswali yoyote kutoka kwa washiriki. Mwishoni atahitimisha mada.

## Nukuu za Mkufunzi

Ukatili wa kijinsia ni ukatili unaoathiri jinsi fulani kwa kiwango kikubwa kuliko jinsi nyingine.

Nchini Tanzania, asilimia 40% ya wanawake wenye umri wa miaka15-49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili, huku asilimia 17% wakifanyiwa ukatili wa kijinsia katika maisha yao. Kati ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49, asilimia 44% wamepitia unyanyasaji wa kimwili au wa kijinsia na wapenzi wao wa karibu.

Unyanyasaji wa wenzi wa ndoa ni mkubwa zaidi katika maeneo ya vijijini, ambapo kwa vijijini ni wastani wa asilimia 52%, wakati matukio ya mjini ni wastani wa asilimia 45%. Takriban asilimia 30% ya wasichana hufanyiwa ukatili wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18.

**(Chanzo: Benki ya Dunia 2022)**

## Aina za Ukatili wa Kijinsia

✓ Ukatili wa kimwili
✓ Ukatili kwa njia ya maneno
✓ Ukatili wa kisaikolojia na kihisia
✓ Ukatili wa kingono
✓ Ukatili wa Kiuchumi

### *a) Ukatili wa Kimwili*

→ Ukatili wa kimwili unahusisha vitendo kama: vipigo, kuunguzwa, kung'atwa, kupigwa mateke na kuuawa.

→ Ukatili wa kimwili pia unahusisha kutendewa ukatili kwa kutumia vitu au silaha mbalimbali kama vile visu, mapanga, shoka, bastola, bunduki n.k.




→ Ukatili wa kimwili ni tendo linalokusudia kusababisha au kuleta maumivu na majeraha katika mwili.



## *b) Ukatili kwa Njia ya Maneno*

→ Ukatili kwa njia ya maneno ni ukatili unaotumia maneno, picha, hotuba, vikaragosi, video na aina nyingine kwa madhumuni ya kuita, kushambulia, kudhalilisha, kutoa vitisho na kumdhibiti mtu mwingine.


→ Pia ukatili kwa njia ya maneno unaweza kufanyika kwa njia ya kukaripia kwa sauti ya juu au ya chini, kuapiza na kutishia.



## *c) Ukatili wa Kisaikolojia na Kihisia*

→ Ukatili wa kisaikolojia ni tendo linalofanywa kwa nia ya kuharibu afya ya kisaikolojia ya mtu mwingine kwa njia ya vitisho au amri.


→ Ukatili wa kisaikolojia unafanyika kwa njia mbalimbali kama vile kumuita mtu majina ya kumdhalilisha mbele za watu, kutishia kumuumiza mtu au watu wake wa karibu, na matendo mengine yenye lengo la kudidimiza afya ya akili ya mhanga.



## d) Ukatili wa Kingono

→ Ni kitendo cha kingono ambacho kinafanyika pasipo ridhaa ya upande mmoja. Baadhi ya vitendo vinavyotendeka kwenye ukatili wa kingono ni pamoja na:

- ✓ Uonevu na vitisho
- ✓ Kudanganya
- ✓ Kutumia nguvu
- ✓ Ubakaji
- ✓ Unyanyasaji wa kingono kwa watoto.
- ✓ Mashambulizi ya kingono.






Mkufunzi anaweza kutoa mfano mwingine wa ukatili wa kijinsia kwa kuwaonesha washiriki filamu inayogusia swala la ukeketaji kwa watoto wa kike.

Filamu hii inapatikana kupitia linki ifuatayo:
*https://www.youtube.com/watch?v=xt3XdU0Fddo.*

### e) *Ukatili wa Kiuchumi*

→ Ukatili wa kiuchumi ni ukatili ambao unajumuisha kuchukua au kupora mapato ya mhanga, kutomruhusu mtu kuwa na kipato chake binafsi, au kumfanya mtu ashindwe kufanya kazi kwa njia ya kumuumiza kimwili. Ni kitendo au tabia yoyote yenye lengo la kusababisha madhara ya kiuchumi kwa mtu.




**Mifano ni kama:** Wanawake wengi katika jamii zetu ni wazalishaji (katika kilimo na ufugaji) lakini wanaume ndio wenye mamlaka na mauzo na mapato yote.

Pia katika jamii fulani hususani vijijini, wanawake hufanya biashara lakini wanalazimika kukabidhi mauzo yote kwa wanaume.

# MADA YA TANO:

# DHANA ZA MSINGI KUHUSU UWEZESHWAJI WA WANAWAKE NA WASICHANA

Uwezeshwaji wa wanawake ni kitendo cha kuwapa wanawake uhuru na utawala juu ya maisha yao na kupata uwezo wa kufanya maamuzi sahihi.

## Malengo ya Mada:

Mara baada ya kumaliza mada hii, kila mshiriki ataweza:

a) Kueleza dhana za msingi kuhusu uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.
b) Kufafanua mambo ya msingi yaliyopo kwenye uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.

## Utangulizi

Mkufunzi atawaongoza washiriki kuandika matarajio yao kuhusu mada itakayofundishwa.

## Tathmini/Kazi ya Awali

Mkufunzi atawaongoza washiriki kubungua bongo kuhusu maana ya uwezeshwaji wa wanawake na wasichana, na maeneo makubwa ya uwezeshwaji huo.

## Uwasilishaji

1) Washiriki watawasilisha majibu waliyopata kwenye majadiliano ya vikundi.
2) Mkufunzi atafafanua na kuongezea maelezo ya ziada kuhusu mambo muhimu na maeneo makubwa ya uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.

## Mazoezi

Washiriki watajadili ni kwa kiwango gani uwezeshwaji wa wanawake na wasichana unafanyika katika jamii zetu na kwa njia zipi.

## Upimaji na Tathmini Baada ya Mafunzo

Mkufunzi atauliza maswali ya papo kwa papo

## Tafakari

Mkufunzi atawaongoza washiriki kutafakari mafanikio na changamoto za uwezeshwaji wa wanawake na wasichana katika jamii zetu.

## Hitimisho

Mkufunzi atatoa muhtasari mfupi wa mada zilizofundishwa, na kujibu maswali yoyote kutoka kwa washiriki. Mwishowe, atahitimisha mada.

## Nukuu za Mkufunzi

**Mambo Muhimu Kuhusu Uwezeshwaji wa Wanawake na Wasichana.**

Uwezeshwaji wa wanawake ni kitendo cha kuwapa wanawake nguvu na utawala juu ya maisha yao na kupokea uwezo wa kufanya maamuzi sahihi.

Uwezeshwaji wa wanawake ni suala muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia, na unahusisha: kupanua wigo wa wanawake kujitambua, uwezo wa kufanya maamuzi, uwezo wa kufikia fursa na rasilimali, uwezo na mamlaka juu ya maisha yake (ndani na nje ya familia), na uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii.



**Maeneo makubwa ya uwezeshwaji wa wanawake ni pamoja na:**

- ✓ Hali ya wanawake kujitambua.
- ✓ Haki ya kuwa na maamuzi.
- ✓ Haki ya kufikia fursa na rasilimali.
- ✓ Haki ya kuwa na uwezo wa kuyatawala maisha yao: ndani na nje ya familia.
- ✓ Uwezo wa kushawishi mwelekeo wa mabadiliko ya kijamii na kutengeneza wigo mpana katika masuala ya jamii, uchumi wa kitaifa na kimataifa.

# MADA YA SITA:

# AINA ZA UWEZESHWAJI WA WANAWAKE NA WASICHANA

## Malengo ya Mada:

Mara baada ya kumaliza mada hii, kila mshiriki ataweza:

a) Kufafanua aina mbalimbali ya uwezeshwaji wa wanawake na wasichana
Kutathmini ubora wa aina mbalimbali ya uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.

## Tathmini/Kazi ya Awali

Mkufunzi atawaongoza washiriki kutaja aina mbalimbali za uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.

## Utangulizi

1) Washiriki watawasilisha majibu yao kuhusu aina mbalimbali za uwezeshwaji wa wanawake na wasichana zilizopo nchini Tanzania.
2) Mkufunzi ataongoza majadiliano na kuongeza maarifa zaidi kuhusu aina za uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.

## Mazoezi

Washiriki watakaa kwenye jozi na kuelezana kwa zamu aina mbalimbali za uwezeshwaji wa wanawake na wasichana.

## Upimaji na Tathmini Baada ya Mafunzo

Mkufunzi atauliza maswali kuhusu aina za uwezeshwaji wa wanawake na wasichana zilizopo Tanzania.

## Tafakari

Mkufunzi atawaongoza washiriki kutafakari juu ya ubora wa aina mbalimbali za uwezeshwaji wa wanawake nchini Tanzania.

## Hitimisho


Mkufunzi atatoa muhtasari mfupi wa mada zilizofundishwa, na kujibu maswali yoyote kutoka kwa washiriki. Mwishoni, atahitimisha mada.

## Nukuu za Mkufunzi

### Aina za Uwezeshwaji wa Wanawake


***a) Uwezeshwaji wa Kijamii***

Hii inahusiana na mifumo wezeshi inayoimarisha mahusiano ya wanawake kijamii na nafasi zao katika mifumo ya kijamii.





***b) Uwezeshwaji wa Kielimu***

Elimu humuweka kila mmoja katika nafasi sawa na kuwawezesha wasichana wadogo kuelewa haki na wajibu wao. Pia, uwezeshwaji wa kielimu unaharakisha upatikanaji wa maarifa ambayo yatainua ujasiri, kujitambua na kuwawezesha wasichana kujiamini.





***c) Uwezeshwaji wa Kiuchumi***

Hii inahusiana na kitendo cha kuwajengea wanawake uwezo wa kufikia kipato, umiliki, utawala na faida katika mapato ya kiuchumi na uwezo wa kufanya maamuzi katika uchumi.



***d) Uwezeshwaji wa Kisiasa***
Hizi ni juhudi zilizolenga kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika jukwaa la siasa na katika maeneo mengine ya kufanya maamuzi ya kisera.




***e) Uwezeshwaji wa Kisaikolojia***
Aina hii ya uwezeshwaji huwasaidia wanawake kuhimili mila na mifumo potofu, na taratibu nyingine za kijamii zinazowabana kubadilisha fikra na mitazamo yao.

